JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA BAJETI YA OFISI YA RAIS – TAMISEMI, OFISI ZA WAKUU WA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

Imetayarishwa na:
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
Mji wa Serikali - Mtumba
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

Julai, 2022

1. UTANGULIZI

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Mpango na Bajeti ya Fungu 56 - Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Fungu Namba 2 - Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 hadi 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020, Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakati wa kulihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Miongozo ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Sera za Kisekta, Mipango Mikakati ya Taasisi husika, Maelekezo na Ahadi mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2022/23.

Mpango huu umezingatia pia, Hati ya Majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, miundo mipya ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Januari, 2022 ambayo ni pamoja na kusimamia: Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D); Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Uratibu wa Uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari; Uratibu na Usimamizi wa Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe, Uratibu wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Uratibu wa masuala ya michezo katika Mamlaka za Serikali za mitaa, Uratibu wa Usafiri Vijijini na Mijini, Usafi wa Mazingira; Uratibu wa Masuala ya Utawala Bora; Uratibu wa shughuli za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC); Uratibu wa Taasisi za Shirika la Elimu Kibaha (KEC); Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI); Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA); Wakala Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART); Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa(LGLB); Usimamizi wa Programu na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

2.0 MUHTASARI WA MPANGO NA BAJETI KWA OR-TAMISEMI, OFISI ZA WAKUU WA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

2.1 Makusanyo ya Maduhuli na Mapato ya Ndani

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Mafungu 28 chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI, yanakadiria kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani ya jumla ya **Shilingi trilioni 1.07** ukilinganisha na bajeti ya kukusanya **Shilingi bilioni 916.44** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 154.23** kama inavyoonesha kwenye **jedwali.**

Jedwali: Muhtasari wa Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 kwa Mafungu 28 ya OR-TAMISEMI

OFISI/TAASISI	MAKADIRIO 2021/22	MAKADIRIO 2022/23	ONGEZEKO	Asilimia
OR-TAMISEMI	52,366,725,886.50	58,145,905,469.50	5,779,179,583.00	11
Mikoa	220,683,312.00	249,281,312.00	28,598,000.00	13
Halmashauri	863,858,000,000.00	1,012,286,089,000	148,428,089,000.00	17

Jumla Kuu	**916,445,409,198.50**	**1,070,681,275,781.50**	**154,235,866,583.00**	**17**

NB: Sababu za kuongezeka kwa Maduhuli na Mapato ya Ndani ni pamoja na usimamizi wa karibu wa OR – TAMISEMI na Mikoa katika ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato hayo, kuongezeka kwa Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki, Ubunifu wa Mhe. Waziri wa Nchi(T) katika kuzishindanisha Halmashauri, Ubunifu wa Vyanzo vipya na kuboresha Mikakati ya kukusanya kwa Halmashauri.

2.2 Muhtasari wa Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Mafungu 28 ya OR-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Mafungu 28 ya OR-TAMISEMI yameidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 8.77** ukilinganisha na **Shilingi trilioni 8.56** kwa bajeti ya mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 210.00** kama inavyoonesha kwenye jedwali.

Jedwali la Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23

Kasma	OR – TAMISEMI	Mikoa	Halmashauri	Tume ya Walimu	Jumla
Matumizi Mengineyo					
Mishahara	63,380,500,000.00	76,205,297,000.00	4,478,391,778,000.00	6,608,202,000.00	4,624,585,777,000.00
Matumizi Mengineyo	14,997,954,000.00	79,099,078,000.00	783,916,091,000.00	8,276,293,000.00	886,289,416,000.00
Jumla Matumizi ya Kawaida	**78,378,454,000.00**	**155,304,375,000.00**	**5,262,307,869,000.00**	**14,884,495,000.00**	**5,510,875,193,000.00**
Miradi ya Maendeleo					
Maendeleo Ndani	770,574,969,000.00	66,018,770,000.00	1,321,771,566,000.00	470,000,000.00	2,158,835,305,000.00
Maendeleo Nje	124,312,896,000.00	18,508,243,000.00	977,485,060,000.00	0	1,120,306,199,000.00
Jumla Maendeleo	**894,887,865,000.00**	**84,527,013,000.00**	**2,299,256,626,000.00**	**470,000,000.00**	**3,279,141,504,000.00**
Jumla kuu	**973,266,319,000.00**	**239,831,388,000.00**	**7,561,564,495,000.00**	**15,354,495,000.00**	**8,779,838,763,200**

2.3 Vipaumbele vya OR – TAMISEMI

Katika Mwaka wa fedha 2022/23 Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i) Uratibu wa shughuli za utawala bora, demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);
ii) Uratibu wa usimamizi wa utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iii) Uratibu na usimamizi wa utoaji wa Elimu Msingi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa ElimuMsingi Bila Malipo;
iv) Uratibu na usimamizi wa Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
v) Uratibu wa ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya Barabara, Afya ya Msingi, Elimu ya Msingi na Sekondari inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
vi) Uratibu na usimamizi wa miradi yote ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vii) Uratibu wa ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, na Halmashauri;
viii) Usimamizi wa matumizi ya rasilimali Watu na fedha katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;
ix) Uendelezaji rasilimali watu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kuwaongezea ujuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;
x) Uwezeshaji wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya uanzishwaji wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji hasa katika Kilimo, Uvuvi na Ufugaji;
xi) Usimamizi wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi zilizochini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xii) Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xiii) Usimamizi wa matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;
xiv) Usimamizi wa utekelezaji wa muundo uliohuishwa wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri wa Januari, 2022;
xv) Uratibu wa masuala ya michezo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Miko ana Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xvi) Uratibu wa usimamizi wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya asilimia 10 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

2.3.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya OR - TAMISEMI

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Ofisi ya Rais –TAMISEMI pamoja na Taasisi zake imeidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 58.14** ikilinganishwa na bajeti ya kukusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 52.36** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 5.77** kama inavyoonekana katika **jedwali**

Jedwali la Muhtasari wa Makadirio ya Maduhuli

OFISI/TAASISI	BAJETI 2021/22	BAJETI 2022/23	Ongezeko/ Upungufu
OR-TAMISEMI	4,500,000.00	-	0
Jumla Ndogo	**4,500,000.00**	**0.00**	-4,500,000.00
Taasisi			
KEC	4,427,543,000.00	4,341,953,000.00	-85,590,000.00
DART	4,768,836,700.00	10,986,269,522.00	6,217,432,822.00
LGTI	9,055,627,005.00	9,757,074,400.00	701,447,395.00
LGLB	3,663,155,634.00	2,613,545,000.00	-1,049,610,634.00
TARURA	30,447,063,547.50	30,447,063,547.50	0.00
Jumla Ndogo Taasisi	**52,362,225,886.50**	**58,145,905,469.50**	5,783,679,583.00
Jumla Kuu	**52,366,725,886.50**	**58,145,905,469.50**	**5,779,179,583.00**

i). Ofisi ya Rais -TAMISEMI Makao Makuu haijakadiria kukusanya maduhuli yoyote kwa sababu ya kuanzishwa kwa mifumo ya TANePS na GePG ambayo malipo yanayokusanywa yanapokelewa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na PPRA.
ii). Makadiro ya mapato ya Shirika la Elimu Kibaha yamepungua kutokana na jengo la hospitali lililokuwa limepangishwa kwa NHIF Mkoa limerudishwa kwa

matumizi ya Shirika na huduma ambazo zilikuwa zinatolewa na hospitali haswa za ufuaji wa mashuka kutoka hospital zingine kusimama baada ya mlipuko wa UVIKO haya yote yamepelekea Shirika kupunguza makadirio ya mapato

iii). Wakala umefanikiwa kuongeza wigo wa mapato kwa kusimika Mfumo wa DART Acecc Fees ambao unakusanya **Shilingi Milioni 20.0** kwa siku badala ya **Shilingi Milioni 8.1** iliyokuwa ikikusanywa awali. Aidha Wakala umebuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato (Kupangisha mabenki na watoa huduma mbalimbali ikiwemo maegesho ya magari na Vendor Machine ya kutolea maji eneo la Kariakoo - Gerezani.

2.3.2 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya OR-TAMISEMI Mwaka wa Fedha 2022/23 na Taasisi zake

Katika Mwaka wa fedha 2022/23, OR-TAMISEMI imeidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 973.26** kama inavyoonesha kwenye **jedwali**

Jedwali la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya OR – TAMISEMI kwa mwaka 2022/23 na Taasisi zake.

Kasma	Bajeti 2021/22 iliyoidhinishwa	Bajeti 2022/23	Badiliko	Asilimia
Mishahara	57,514,498,000.00	63,380,500,000.00	5,866,002,000.00	10
Matumizi Mengineyo	11,373,154,000.00	14,997,954,000.00	3,624,800,000.00	32
Jumla ya Matumizi Kawaida	**68,887,652,000.00**	**78,378,454,000.00**	**9,490,802,000.00**	14
Maendeleo Ndani	773,664,968,800.00	770,574,969,000.00	-3,089,999,800.00	0
Maendeleo Nje	200,155,403,132.00	124,312,896,000.00	-75,842,507,132.00	-38
Jumla ya Fedha za Maendeleo	**973,820,371,932.00**	**894,887,865,000.00**	**-78,932,506,932.00**	-8
Jumla Kuu OR - TAMISEMI	**1,042,708,023,932.00**	**973,266,319,000.00**	**-69,441,704,932.00**	-7

2.4 Vipaumbele vya Ofisi za Wakuu wa Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

Katika Mwaka wa fedha 2022/23 Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i) Usimamizi wa masuala ya ulinzi na usalama katika Mikoa na Wilaya;
ii) Uimarishaji wa utawala bora, uwajibikaji na uwazi kwa kufanya Vikao vya vyote vya kisheria;
iii) Uratibu wa usimamizi wa utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iv) Uratibu na usimamizi wa utoaji wa Elimu Msingi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa ElimuMsingi Bila Malipo;
v) Usimamizi wa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri;
vi) Utambuzi wa maeneo na uwekaji wa alama za mipaka za Mikoa, Wilaya na Tarafa;

vii) Uratibu na usimamizi wa Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
viii) Uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri;
ix) Uimarishaji wa Kamati za Bajeti za Mikoa ili kuhakikisha zinaandaa na kusimamia mpango na bajeti ya Mikoa na Halmashauri,
x) Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi ya Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Watumishi;
xi) Uendelezaji rasilimali watu katika Mikoa kwa kuwaongezea ujuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuwawezesha kutoa ushauri wa kitaalam kwa watumishi wa Serikali za Mitaa;
xii) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya fedha za Serikali kuu, mapato ya ndani na wadau katika Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na TARURA;
xiii) Uratibu wa majukum ya usajili na usimamizi wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha;
xiv) Uwezeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya uanzishaji wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika sekta za uchumi za uzalishaji na fursa nyingine zilizopo katika maeneo yao;
xv) Uratibu na usimamia wa Halmashauri kuhusu ufanikishaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

2.4.1 Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa Mwaka wa Fedha 2022/23

2.4.2 Makusanyo ya Maduhuli

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zimeidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi milioni 249.28** ikilinganishwa na **Shilingi milioni 220.68** kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambapo makadirio yameongezeka kwa **asilimia 13.**

2.4.3 Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Bajeti ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa Mwaka wa Fedha 2022/23

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Mikoa imeidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 239.83** kiasi hiki kimepungua kwa **asilimia 1** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22 kama inavyoonesha kwenye **jedwali**

Jedwali la Muhtasari wa Mpango na Bajeti ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa kwa Mwaka 2022/23

Kasma	Bajeti 2021/22	Bajeti 2022/23	Badiliko	Asilimia
Mishahara	71,269,064,000.00	76,205,297,000.00	4,936,233,000.00	7
Matumizi Mengineyo	57,449,078,000.00	79,099,078,000.00	21,650,000,000.00	38
Jumla ya Matumizi Kawaida	**128,718,142,000.00**	**155,304,375,000.00**	26,586,233,000.00	21
Maendeleo Ndani	90,328,294,134.00	66,018,770,000.00	-24,309,524,134.00	-27
Maendeleo Nje	23,798,684,480.00	18,508,243,000.00	-5,290,441,480.00	-22
Jumla ya Fedha za Maendeleo	**114,126,978,614.00**	**84,527,013,000.00**	-29,599,965,614.00	-26

Jumla Kuu Mikoa	**242,845,120,614.00**	**239,831,388,000.00**	**-3,013,732,614.00**	-1

2.5 Vipaumbele vya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

Katika Mwaka wa fedha 2022/23 Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i) Usimamizi wa masuala ya ulinzi na usalama;
ii) Uboreshaji wa huduma za afya, lishe na ustawi wa jamii na usafi wa mazingira katika vituo vya kutoa huduma za afya na ngazi ya jamii;
iii) Uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari;
iv) Uimarishaji na usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri;
v) Uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;
vi) Uimarishaji wa utawala bora na uwajibikaji;
vii) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya fedha za serikali kuu, mapato ya ndani na wadau;
viii) Uimarishaji wa Kamati za Bajeti za Halmashauri ili kuhakikisha zinaandaa na kusimamia mpango na bajeti,
ix) Uimarishaji wa miundombinu ya barabara za mijini na vijijini;
x) Usimamizi wa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri;
xi) Uwekaji wa mazingira wezeshi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa vikundi vya Watu Wenye Ulemavu, Vijana na Wanawake;
xii) Utengaji wa maeneo na kuweka miundombinu wezeshi kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo (Wamachinga) na kuwapatia elimu ya biashara na ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za fedha na masoko ili kukuza fursa za ajira na uchumi wa maeneo husika;
xiii) Uboreshaji wa huduma ndogo za fedha kwa kuimarisha Kamati za Usimamizi katika usajili, kujenga uwezo wa vikundi vya fedha vya kijamii pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini;
xiv) Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi ya Viongozi na Watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xv) Utengaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi za ngazi ya msingi
xvi) Mapitio, marekebisho na utungaji wa Sheria Ndogo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na Utawala Bora;
xvii) Utatuzi wa migogoro ya ardhi, uendelezaji wa mipango miji na matumizi bora ya ardhi;
xviii) Uimarishaji wa huduma za ugani kwa kutekeleza programu za kilimomazao, kilimomifugo na kilimouvuvi;
xix) Uendelezaji wa ushirika pamoja na uwekaji wa mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika;
xx) Usimamizi wa mazingira;
xxi) Usimamizi wa utekelezaji wa Muundo wa Halmashauri uliohuishwa Januari 2022;

xxii) Kuweka mazingira mazuri ya uanzishwaji wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Wadau wote; na

xxiii) Usimamizi wa michezo na uibuaji wa Vipaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

2.6 Mapato ya ndani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

2.6.1 Mapato ya Ndani

Katika mwaka wa fedha 2022/23 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeidhinishiwa kukusanya Mapato ya Ndani ya jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 863.85** iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Makadirio ya Mapato ya Ndani yameongezeka kwa **Shilingi bilioni 148.42** kwa Mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la **asilimia 17.**

2.6.2 Muhtasari wa Mpango na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2022/23

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeidhinishiwa kukusanya, kupokea na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 7.56** ukilinganisha na **Shilingi trilioni 7.26** kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 293.52** kama inavyoonesha kwenye **jedwali.**

Jedwali la Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Mwaka wa Fedha 2022/23

Kasma	Bajeti 2021/22	Bajeti 2022/23	Ongezeko	Asilimia
Mishahara	3,835,605,473,000.00	4,478,391,778,000.00	642,786,305,000.00	17
Matumizi mengineyo(SK)	147,659,832,000.00	166,430,744,000.00	18,770,912,000.00	13
Matumizi mengineyo(OS)	532,768,338,000.00	617,485,347,000.00	84,717,009,000.00	16
Jumla ya Matumizi Kawaida	**4,516,033,643,000.00**	**5,262,307,869,000.00**	746,274,226,000.00	17
Maendeleo Ndani(SK)	957,510,351,000.00	926,970,824,000.00	-30,539,527,000.00	-3
Maendeleo Ndani(OS)	331,089,662,000.00	394,800,742,000.00	63,711,080,000.00	19
Maendeleo Nje	1,463,406,365,224.00	977,485,060,000.00	-485,921,305,224.00	-33
Jumla ya Fedha za Maendeleo	**2,752,006,378,224.00**	**2,299,256,626,000.00**	-452,749,752,224.00	-16
Jumla Kuu	**7,268,040,021,224.00**	**7,561,564,495,000.00**	**293,524,473,776.00**	**4**

2.7 Vipaumbele vya Tume ya Walimu

Katika Mwaka wa fedha 2022/23 Tume ya Utumishi wa Walimu inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i) Kusimamia utumishi na maendeleo ya Walimu kwa kudumisha Maadili na Nidhamu kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Utumishi wa Umma, Kuhakikisha kwamba Walimu wenye sifa wanapandishwa vyeo kwa wakati baada ya kibali kutolewa na Mamlaka husika;

ii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume Makao Makuu;

iii) Kufuatilia uteuzi wa Makatibu Wasaidizi ngazi ya Wilaya ili kuweza kutekeleza kikamilifu Muundo wa Tume.

iv) Kuimarisha Mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Masuala ya Walimu;

v) Kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa Tume kwa kuwaongezea ujuzi, kuwapatia ofisi na vitendeakazi; na

vi) Kuongeza uelewa kwa Wadau kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu.

2.7.1 Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu Mwaka wa Fedha 2022/23

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Tume ya Utumishi wa Walimu imeidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 15.35** kiasi hiki ni ongezeko kwa **Shilingi milioni 485.72** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka 2019/20 kama inavyoonekana katika **jedwali.**

Jedwali Na. 14: Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa Mwaka 2022/23

Kasma	Bajeti 2021/22	Bajeti 2022/23	Badiliko	Asilimia
Mishahara	7,760,568,000	6,608,202,000.00	-1,152,366,000.00	-15
Matumizi Mengineyo	6,608,202,000	8,276,293,000.00	1,668,091,000.00	25
Miradi ya Maendeleo	500,000,000.00	470,000,000.00	-30,000,000.00	-6
Jumla	**14,868,770,000.00**	**15,354,495,000.00**	**485,725,000.00**	**3**

MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA NA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/23

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imepanga kutekeleza malengo mahsusi yafuatayo: -

Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo

(i) Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo umeongezewa **Shilingi bilioni 4.99** kutoka **Shilingi bilioni 11.00** iliyokuwa katika bajeti ya kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 - 2021/22 hadi **Shilingi bilioni 15.99** kwa mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la **asilimia 45.36** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi;

Mchango wa Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Madiwani

(ii) Serikali ilianza kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo mchango wa bima ya afya haukujumuishwa kwenye posho hizo. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, Serikali imetenga fedha ya kuchangia mchango wa mwajiri kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani **Shilingi milioni 607.57**;

Kuimarisha Usalama na Usimamizi wa Shughuli za Serikali

(iii) Mikoa imeongezewa fedha za uendeshaji wa vikao vya Kamati za Usalama vya mikoa kutoka **Shilingi milioni 416.00** hadi **Shilingi milioni 780.00** sawa na ongezeko la **Shilingi milioni 364.00**;

(iv) Mikoa **12** inayopakana na nchi jirani imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 730.00** kwa ajili ya kuimarisha usalama mipakani;

(v) Ofisi za Wakuu wa Wilaya zimeongezewa fedha za matumizi mengineyo kutoka **Shilingi bilioni 17.13** hadi **Shilingi bilioni 26.68** sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 9.55** ambalo ni ongezeko la **asilimia 55.75** kwa ajili ya

kuwawezesha kusimamia usalama na utekelezaji wa shughuli za Serikali katika maeneo yao;

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

(vi) Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imetengewa **Shilingi bilioni 802.29** kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara ambapo barabara za lami zenye urefu wa kilomita **411.80**, changarawe urefu wa kilomita **10,666.11,** ujenzi wa mifereji ya maji yenye urefu wa **mita 12,542.50,** matengenezo ya barabara **kilomita 24,015.77** na madaraja na vivuko **322** vitajengwa. Aidha, TARURA itaanza taratibu za ununuzi mwezi Mei, 2022 ya **asilimia 60** ya kazi zilizopangwa ili utekelezaji ufanyike kwa wakati;

Mapato ya Ndani na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

(vii) Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya Mapato ya Ndani ya jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 863.85** zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ni ongezeko la **Shilingi bilioni 148.42** sawa na **asilimia 17.18**. Ongezeko hili limetokana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati ya pamoja ya kubuni vyanzo vipya, kuimarisha vilivyopo na mikakati zaidi ya ukusanyaji wa mapato;

(viii) **Shilingi bilioni 394.80** zimetengwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 75.98** ni mikopo ya **asilimia 10** na **Shilingi bilioni 318.82** ni kwa ajili ya miradi mingine ya maendeleo kama ifuatavyo:- **Shilingi bilioni 35.32** zitatumika kuboresha miundombinu ya afya. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa wa Hospitali **6** za Halmashauri, vituo vya afya **101,** zahanati **205,** vituo vya kukusanyia taka **59,** majengo ya huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD) katika vituo vya afya na Hospitali **9** pamoja na huduma za lishe na ununuzi wa madawa; **Shilingi bilioni 25.89** zitatumika kuboresha miundombinu ya biashara ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa stendi **74**, masoko **110,** maegesho ya magari **38,** kuweka mazingira wezeshi ya viwanda vidogo **26,** maeneo ya kupumzikia **4** pamoja na kuboresha vituo vya kukusanyia mapato **61; Shilingi bilioni 51.52** zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vyumba vya madarasa **2,935,** matundu ya vyoo **4,787,** daharia (hosteli) **102**, maabara za masomo ya sayansi **78,** mabwalo ya chakula **20** na kutengeneza madawati **56,049; Shilingi bilioni 7.57** zitatumika kuboresha miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa machinjio **124,** miundombinu ya umwagiliaji **50,** maghala **12,** majosho **52**, mashamba darasa **28,** mabwawa ya samaki **31**, malambo **10** na mashine za usindikaji **8; Shilingi bilioni 93.71** zitatumika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi ikiwemo ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala yakijumuisha ofisi za walimu na ofisi za Halmashauri **482,** nyumba za watumishi **303**, uzio wa majengo **87,** ofisi za kata **113,** kumbi **30,** ofisi za vijji **98,** ofisi za Mitaa **16,** ununuzi wa pikipiki **65,** malori **manne (4),** ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa mafunzo, mifumo ya umeme na TEHAMA; **Shilingi bilioni 13.32** zitatumika kwa ajili ya mipango miji na matumizi bora ya ardhi, vituo vya utalii na viwanja vya michezo; na **Shilingi bilioni 21.95** zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara, madaraja **20,** uwekaji wa

taa za barabarani na ujenzi wa mifereji ya maji; na **Shilingi bilioni 68.99** zimepangwa kutumika katika miradi mingine;

(ix) **Shilingi bilioni 75.97** zinazotokana na **asilimia 10** ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri ambayo ni sehemu ya miradi ya maendeleo zimetengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambayo ni sehemu ya fedha za maendeleo zinazotokana na asilimia 40/60. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 30.39** ni kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, **Shilingi bilioni 30.39** ni kwa ajili ya vikundi vya Vijana na **Shilingi bilioni 15.19** ni kwa ajili ya vikundi vya Watu Wenye Ulemavu.
Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha mikopo hii inasimamiwa kwa ufanisi. Moja ya mikakati iliyowekwa ni kuweka kigezo cha utoaji wa mikopo, usimamizi wa matumizi ya mikopo hiyo pamoja na marejesho kuwa sehemu ya kuwapima Wakurugenzi wa Halmashauri ambayo itafanyika kila robo mwaka na tathmini ya kina itafanyika mwisho wa mwaka. Mkakati mwingine ni matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki utakaosaidia kuondoa changamoto katika ukopeshaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo. Hivyo, itakuwa ni kazi ya Wakurugenzi kuhakikisha mfumo unatumika ipasavyo na kuongeza ufanisi; na

(x) Jumla ya **Shilingi bilioni 4.76** zimetengwa kwa ajili ya uratibu wa Huduma Ndogo za Fedha ambapo Taasisi na vikundi vinavyojishughulisha na shughuli za fedha ambavyo siyo rasmi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa vitarasimishwa kupitia utaratibu huu;

Sekta ya Afya

(i) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali **28** za Halmashauri ambazo zimeidhinishwa **Shilingi bilioni 24.65**;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali **31** za Halmashauri ambazo zimeidhinishwa **Shilingi bilioni 15.50**;

(iii) Ukarabati wa Hospitali kongwe **19** za Halmashauri ambazo zimeidhinishwa **Shilingi bilioni 16.55;**

(iv) Ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya Zahanati **300** ambazo zimeidhinishwa **Shilingi bilioni 15.00**;

(v) **Shilingi bilioni 15.15** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba kwa Zahanati **300, Shilingi bilioni 47.70** za ununuzi wa Vifaa Tiba kwa Vituo vya Afya **159** na **Shilingi bilioni 7.10** za ununuzi wa Vifaa Tiba ya afya ya kinywa na macho kwa ajili ya hospitali za Halmashauri **71** zilizokamilika;

Sekta ya Elimu

(vi) Elimumsingi Bila Malipo kiasi cha **Shilingi bilioni 346.49** zimetengwa sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 34.44** ya fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2021/22 ambayo ni **Shilingi bilioni 312.05**;

(vii) **Shilingi bilioni 55.57** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **809** za walimu zenye uwezo wa kuchukua kaya **1,916**. Kati yake, nyumba za walimu wa shule za msingi ni **298** za **(3 in1)** ambazo zitajengwa kupitia fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa **Shilingi bilioni 30.02** na **Shilingi bilioni**

25.55 zitatumika kujenga nyumba **511 (2 in1)** za walimu wa shule za sekondari kupitia mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**;**

(viii) Ujenzi wa matundu ya vyoo **9,700** katika Vituo shikizi **970** ambapo **Shilingi bilioni 10.67** zimetengwa;

(ix) Kuanza Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **1,700** katika Shule Kongwe za Msingi **Shilingi bilioni 34.00** zimetengwa**;**

(x) Ujenzi wa Shule Mpya **39** za Msingi **Shilingi bilioni 15.60** zimetengwa**;**

(xi) Ujenzi wa uzio wa mabweni **99** ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo **Shilingi bilioni 2.97** zimetengwa**;**

(xii) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa **1,911** katika Shule za Msingi ambapo **Shilingi bilioni 23.88** zimetengwa**;**

(xiii) Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara **291** katika Shule za Sekondari ambapo **Shilingi bilioni 8.73** zimetengwa;

(xiv) Ukamilishaji wa mabwalo **86** ambapo mabwalo **80** katika shule za sekondari na mabwalo **sita (6)** katika Shule za Msingi **Shilingi milioni 4.30** zimetengwa**;**

(xv) Ukamilishaji wa mabweni **461** ambapo mabweni **28** katika shule za Msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum na mabweni **433** kwa Shule za Sekondari ambapo **Shilingi bilioni 9.21** zimetengwa**;**

(xvi) Kuwezesha kufanyika kwa mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne, la Saba, Kidato cha Pili, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **Shilingi bilioni 142.33** zimetengwa;

(xvii) **Shilingi milioni 670.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na uundaji wa mfumo;

Utawala Bora

(xviii) Jumla ya **Shilingi bilioni 36.11** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za viongozi kama ifuatavyo: **Shilingi bilioni 1.15** zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 3 ya Dodoma, Kilimanjaro na Singida; **Shilingi bilioni 3.58** kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa **9;** Wakuu wa Wilaya **15** na Ofisi moja (1) ya Afisa Tarafa; **Shilingi milioni 967.89** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba mbili **(2)** za Wakuu wa Mikoa, nyumba **18** za Wakuu wa Wilaya, nyumba moja **(1)** ya Katibu Tawala wa Mkoa na nyumba **4** za Makatibu Tawala wa Wilaya; **Shilingi bilioni 2.38** zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi na ukamilishaji wa Ikulu ndogo saba **(7)** na ukarabati wa Ikulu Ndogo tatu **(3)**; **Shilingi bilioni 6.75** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa nyumba za Viongozi **40**; **Shilingi bilioni 19.43** kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya ofisi **61** yakiwemo ya Wakuu wa Mikoa **10**; Wakuu wa Wilaya **19** na ofisi za Tarafa **32.**

(xix) Serikali imetenga **Shilingi bilioni 10.00** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Soko jipya la Kariakoo na kukarabati Soko Kuu liloungua moto tarehe 10 Julai, 2021;

(xx) Serikali imetenga **Shilingi bilioni 8.90** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **111** za Wakuu wa Idara na **Shilingi bilioni 7.20** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **48** za Wakurugenzi;

(xxi) Halmashauri **83** zimeidhinishwa **Shilingi bilioni 68.85** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala;

(xxii) Halmashauri **13** zimeidhinishwa **Shilingi bilioni 13.00** kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya ya utawala;

(xxiii) Jumla ya **Shilingi bilioni 2.05** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa boti: Halmashauri za Wilaya za Mafia **(boti mbili**), Kilwa (**boti moja**), Ukerewe (**boti mbili**), Muleba (**boti moja**), Kalambo (**boti moja**) na Momba (**boti moja**);

(xxiv) Halmashauri **20** zimeidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 40.11** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati;

Programu mbalimbali

(xxv) Jumla ya **Shilingi bilioni 1.41** zimetengwa kupitia Programu ya Kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuimarisha Mfumo wa Ugatuaji utakaosaidia kuboresha huduma za jamii, utawala bora na kuwa na maendeleo endelevu;

(xxvi) Jumla ya **Shilingi bilioni 135.43** zimetengwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa shule **10** za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi, shule za sekondari **232** za Kata, ujenzi wa shule mpya za kata **184**, ujenzi wa shule mpya **tano (5)** za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi na fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini;

(xxvii) Jumla ya **Shilingi bilioni 55.38** zimetengwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira (SRWSS) kwa upande wa elimu na Afya kwa ajili ya kuimarisha shughuli za afya na usafi wa mazingira;

(xxviii) Jumla ya **Shilingi bilioni 237.36** zimetengwa kupitia Programu ya BOOST kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji katika elimu ya awali na msingi;

(xxix) Jumla ya **Shilingi bilioni 17.27** zimetengwa kupitia DART kwa ajili ya kununua Mfumo wa kusimamia magari na kusimika vifaa vya kukusanyia nauli kwa mfumo wa kielektroniki; na

(xxx) Jumla ya **Shilingi bilioni 83.29** zimetengwa kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma.